# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)2130852
Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz

*Unapojibu tafadhali taja:*
Kumb Na: NBS/S.40/21/477

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe: 07 June, 2013

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI MEI, 2013

## Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Februari 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi-vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMESHUKA HADI ASILIMIA 8.3

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Mei, 2013 (Septemba, 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Mei - 12 | Aprili-13 | Mei-13 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 141.19 | 154.94 | 152.48 | -1.6 | 8.0 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 112.85 | 132.62 | 133.18 | 0.4 | 18.0 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 121.92 | 128.14 | 128.44 | 0.2 | 5.3 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 129.50 | 154.49 | 154.04 | -0.3 | 19.0 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 121.39 | 126.62 | 126.69 | 0.1 | 4.4 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 105.00 | 108.10 | 108.10 | 0.0 | 3.0 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 115.08 | 119.96 | 123.68 | 3.1 | 7.5 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 96.64 | 96.07 | 95.96 | -0.1 | -0.7 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 108.69 | 112.36 | 112.54 | 0.2 | 3.5 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 110.75 | 113.16 | 113.16 | 0.0 | 2.2 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 126.59 | 133.42 | 133.53 | 0.1 | 5.5 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 114.29 | 119.69 | 119.87 | 0.2 | 4.9 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100.0** | **129.92** | **141.59** | **140.76** | **-0.6** | **8.3** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 139.58 | 152.57 | 150.39 | -1.4 | 7.7 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 143.63 | 173.81 | 172.51 | -0.7 | 20.1 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 118.48 | 128.61 | 129.36 | 0.6 | 9.2 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 114.70 | 121.81 | 122.87 | 0.9 | 7.1 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Mei, 2013 umepungua hadi asilimia 8.3 kutoka asilimia 9.4 mwezi Aprili, 2013. Kupungua kwa Mfumuko wa Bei wa mwezi Mei, 2013 kunamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwezi Mei, 2013 imepungua ikilinganishwa na kasi ya kupanda kwa bei kwa mwezi Aprili, 2013. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 140.76 mwezi wa Mei, 2013 kutoka 129.92 mwezi Mei, 2012. Mfumuko wa Bei wa Vyakula na Vinywaji Baridi umepungua hadi asilimia 8.0 mwezi wa Mei, 2013 kutoka asilimia 10.2 kwa mwezi wa Aprili, 2013.

### Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Badiliko la Fahirisi ya Bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limepungua hadi asilimia 7.7 mwezi wa Mei, 2013 ikilinganishwa na asilimia 9.7 mwezi wa Aprili, 2013. Kasi ya ongezeko la bei kwa bidhaa zisizo za vyakula imeongezeka hadi asilimia 9.2 kwa mwezi wa Mei, 2013 kutoka asilimia 8.9 mwezi Aprili, 2013.

## Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa nyumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Mei, 2013 umeongezeka hadi asilimia 7.1 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwezi Aprili, 2013. Mfumuko wa Bei wa Nishati kwa mwezi Mei, 2013 umepungua hadi kufikia asilimia 20.1 ikilinganishwa na asilimia 21.6 mwezi wa Aprili, 2013.

**Kielelezo Namba 1: Mwelekeo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mei, 2012 Hadi Mei, 2013. (Septemba 2010 = 100)**




Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonyesha kuwa, katika kipindi kati ya mwezi Mei, 2012 hadi Mei, 2013, kumekuwa na mwenendo wa kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali kama inavyoonyeshwa na Fahirisi za Bei. Mfumuko wa Bei umekuwa na mwenendo wa kushuka kutoka asilimia 18.2 mwezi Mei, 2012 hadi kufikia asilimia 8.3 mwezi Mei, 2013.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEPUNGUA KWA ASILIMIA 0.6

Mfumuko wa Bei wa mwezi Mei, 2013 umepungua kwa asilimia 0.6 ikilinganishwa na asilimia 0.5 kwa mwezi Aprili, 2013. Fahirisi za Bei zimepungua hadi 140.76 mwezi Mei, 2013 kutoka 141.59 mwezi Aprili, 2013. Kupungua kwa Mfumuko wa Bei kwa kipimo cha mwezi kumechangiwa hasa na kupungua kwa bei za bidhaa za vyakula. Bidhaa za vyakula zilizochangia kupungua kwa mfumuko wa bei kwa kipimo cha mwezi ni pamoja na; mchele kwa asilimia 10.1, mahindi kwa asilimia 4.5, unga wa mahindi kwa asilimia 5.6, unga wa ngano kwa asilimia 2.4, matunda kwa asilimia 2.3, karanga kwa asilimia 7.8, nazi kwa asilimia 7.2, vitunguu maji kwa asilimia 1.1,

mafuta ya kupikia kwa asilimia 0.6, dagaa kwa asilimia 0.6, viazi vitamu kwa asilimia 1.4 na sukari kwa asilimia 1.6.


## Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Septemba, 2010 Ikilinganishwa na Mwezi Mei, 2013

**Tafsiri**: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inatafsiriwa kuwa ni badiliko la Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania ingeweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Fahirisi za Bei za Taifa unaongezeka, Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma hupungua.

Uwezo wa Shilingi 100 ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma umepungua hadi Shilingi 71 na senti 04 kutoka mwezi Septemba, 2010 hadi Mei 2013.

## MIENENDO YA BEI

### Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei Kutoka Mei, 2012 Hadi Mei, 2013. (Septemba 2010 = 100)




Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonyesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei kuanzia mwezi Mei, 2012 hadi mwezi Mei, 2013. Kwa wastani, Fahirisi za nishati na mafuta na Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi zingine. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo za chakula pamoja na nishati zimeonyesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**